
# MWONGOZO WA NOVELA

## "UTEUZI WA CHALE "-Asumpta K Matei.

***Mwalimu  Sudi.G.Hamisi***

***Mwalimu Mzoefu na mwenye tajriba pana katika uwanja wa Jiografia/ Kiswahili lugha na fasihi.***

***B.E.D /Arts  MOI UNIVERSITY.***



## MUKHTASARI.

Uteuzi ni neno linalotokana na neno teua yaani chagua.Chale ni mhusika katika novela hii.Uteuzi wa Chale ni uamuzi ambao mhusika chale alipaswa kuchukua katika kuchagua  kipawa kipi angetumia ili kuitumikia jamii.

Chale ambae ni mwanafunzi wa gredi ya saba anafahamika Kwa umaarufu wake kutokana na kipaji chake cha utangazaji.Yeye hutangaza au hupeperusha matangazo ya michezo ya vijana wanapokuwa wakijumuika pamoja katika michezo hiyo na kuifanya kufana zaidi na yenye mvuto.Wanapokuwa katika mashindano ya kuogelea katika bwawa la Mpingoni,yeye hupeperusha matangazo ya mashindano  hayo ya kuogelea akiwa kwenye jiwe maarufu lililofahamika kama 'Sanduku la mtangazaji'.Aliyapamba mashindano haya nakuyafanya yakuvutia zaidi hadi baadhi ya vijana wenzake wakambandika jina "mtangazaji mtarajiwa".

Siku moja Chale na wenzake wakiwa wametekwa na shughuli za mashindano ya uogeleaji,walijisahau kuwa walifaa kuwatupia jicho ng'ombe na hivyo basi,ngombe hao wakatokomea walikokwenda.Ghafla bin vu walilingundua hili na Ili kuepuka adhabu watoto wenzake wakapiga lundi.Chale alimuona baba yake amefika bwawani lakini hakudhihirisha sura ya hasira.Mbali na hivyo Chale alivaa gwanda lake na kutoka shoti mithili ya risasi.



Edit with WPS Office

Alfajiri iliyofuata Chale aliamka na maumivu makali ya mguu ambayo hata yeye mwenyewe alishindwa kung'amua chanzo chake.Baada ya babake Mzee Jibril na mamake Bi Pili kuona maji yamezidi unga,waliamua kumpeleka mwanao katika kituo Cha afya Cha mwuguzi.Baada ya Daktari kumfanyia vipimo vya joto na vya mguu uliofura,akagundua kuwa joto lilikua juu sana na kuwa mguu ule haukuonyesha dalili yoyote ya kuteguka na hivyo basi akampatia mgonjwa dawa za kupunguza maumivu na kuwapatia barua ya kuwaamuru kuelekea hospitali kuu ya kaunti ili kufanyiwa uchunguzi wa kina.Daktari akawafahamisha kuwa huenda akahitajika kulazwa hospitalini huko Ili kurahisisha vipimo na matibabu jambo ambalo lilimshtua Chale.

Katika hospitali kuu ya kaunti ya Heri wanakutana katika chumba Cha daktari na daktari yuho huyo aliyemhudumia Chale katika kituo Cha afya Cha mwuguzi usiku uliotangulia.Si mwingine bali Daktari Maarifa.Chale alilazwa katika wadi ya st.Bakita Ili kufanyiwa uchunguzi wa kina.katika wadi hiyo mwuguzi wake anakua ni sudi.Baada ya uchunguzi wa kina uliohusisha hadi baadhi ya vipimo kufanyiwa ng'ambo ,Daktari maarifa aliwabainishia wazi kuwa Mwanao Chale alikua na uvimbe kwenye sehemu inayounganisha wayo na muundi na kuwa uvimbe huo ulikuwa na seli za Kansa au saratani na hivyo basi alihitaji upasuaji wa haraka.

Siku ya oparesheni ilipowadia,Daktari Maarifa,na wenzake pamoja na sudi walijumuika katika chumba Cha oparesheni Kwa shughuli iliyotarajiwa.Daktari maarifa aliongoza upasuaji huo ambao uliebuka kuwa wenye ufanisi na Daktari Maarifa akalitoa tufe lililokuwa limejificha kwenye sehemu inayounganisha wayo na muundi.Safari ya kupona ya Chale ikaanzia hapo.Mzee Jibril na Bi Pili walijawa na furaha na ufanisi huo ijapokuwa Jibril alikuwa na hofu kuhusu malipo ya upasuaji kwamba yangekua maradufu.Daktari Maarifa akawahakikishia kuwa gharama yote ya matibabu ilikuwa juu yake jambo lililowafanya kummimina shukrani sufufu.

Baada ya Chale kupona na kutoka hospitalini,alirudi katika shule yake aliyokuwa akisomea kabla ya kuugua.Walimu wakafikia uamuzi wa Chale kuendelea na gredi ya nane ijapokuwa alikuwa hajaisoma kikamilifu gredi ya saba.uamuzi huu uliafikiwa baada ya wao kumhoji Chale na kugundua kuwa  alikua akijiendeleza kimasomo alipokuwa hospitalini.

Chale alikua  na vita vikali kuhusu taaluma ambayo angependa kuiendeleza.Tokea alipopokea msaada mkubwa kutoka Kwa Daktari maarifa,alikua katika njia panda.Hakujua aendelee kupigania talanta yake ya utangazaji aliyoienzi au kujikita katika uwanja wa matibabu aweze kuokoa jamii.



Edit with WPS Office

Simu moja baada ya kupewa kazi ya utafiti shuleni kuhusu mangojwa ambukizi na kuibuka bingwa katika utafiti wake,azma yake ya kusomea taaluma ya matibabu ilikua Kwa Kasi mno.

Chale alijiunga na Chuo kikuu Cha Seraji katika Kitiv o Cha Afya na Tiba.Huko Chuoni anakutana na mwuguzi na rafikiye sudi ambaye amejisajili kuendeleza taaluma yake ya uuguzi.Chale alisomea taaluma ya upasuaji na matibabu ya viungo vya mwili vinavyohusiana na mkojo kama vile Figo,kibofu.

Chale anamfanyia upasuaji daktari wake na rafikiye wa dhati Daktari maarifa aliyekuwa na tatizo la uvimbe kwenye kibofu.Anafanikiwa na kuyaokoa maisha ya daktari maarifa kama vile alivyookolewa maisha yake  awali.Ama kweli wema hauozi.

## UFAAFU WA ANWANI.

Je novela hii inaafiki anwani"uteuzi was Chale?"

Ama kweli novela hii inasadifu anwani  "uteuzi wa Chale" kwa kuwa inamhusu mhusika Chale aliyekuwa na vipawa anuwai.Chale alihitajika kuchagua kipawa ambacho angeweza kukiendeleza katika kuihudumia jamii.Chale alikua na kipawa Cha Uogeleaji,Utangazaji,Utabibu na hata Ualimu Kwa kuwa alikuwa mfafanuzi mzuri wa mambo.Alihitajika kuchagua kipawa kati ya hivi ambacho angeweza kukiendeleza Ili kuhudumia jamii.uteuzi huu ulimhusu yeye mwenyewe.Alipotaka ushauri kutoka Kwa babake,aliambiwa wazi ya kuwa vipawa vyote alivyo navyo ni muhimu ila katika uteuzi wa kipi angetumia ili kuihudumia jamii,ulikuwa mikononi make.Uteuzi ulikua wake,"Uteuzi wa Chale".

## DHAMIRA.

Dhamira ya mtunzi katika novela ya "Uteuzi wa Chale" ni



Edit with WPS Office

kudhihirisha umuhimu wa kuvikuza vipawa kwa manufaa ya baadae na vilevile haja ya kukiteua kipawa mwafaka katika kuihudumia jamii.

## MAUDHUI

1. **UKUZAJI WA VIPAWA.**

Ni muhimu watoto kupewa nafasi na kusaidiwa kuvikuza vipawa vyao mbalimbali.Chale na nduguye wanaruhusiwa na wazazi wao kujihusisha na michezo yao uogeleaji Bwawani ili kukuza vipawa vyao vya uogeleaji.Ni dhahiri shahiri kuwa Mzee jibril anafahamu vyema umuhimu wa kuwasaidia watoto kuvikuza vipawa vyao vitakavyoweza kuwasaidia siku za usoni.Kina Chale wanaposahau kuwachunga ng'ombe malishoni kwasababu ya shughuli zao za uogeleaji,Mzee jibril anakosa kuwaadhibu Kwa kuwa ajijua fika kuwa walichokuwa wakikifanya,ilikua njia moja ya kukuza vipawa vyao jambo ambalo ni muhimu Kwa watoto.

Vile vile,katika shule ya Mfinyanzi,vipawa vya wanafunzi vinakuzwa ipasavyo Kwa njia mbalimbali.Wanafunzi wanapewa kazi ya kutafiti kuhusu mangonjwa ambukizi ambapo Chale anaibuka gwiji katika hili.Kazi za utafiti huweza kukuza vipawa vya watoto.

2. **MABADILIKO YA HALI YA ANGA.**



Edit with WPS Office

Awali bwawa la mpingoni halikuweza kukauka lakini lilianza kukauka kutokana na mabadiliko ya Hali ya anga.Mtunzi anahimiza umuhimu wa kuyahifandhi mazingira Ile kuepuka athari mbaya kutokana na mabadiliko ya Hali ya anga.

3. **UWAJIBIKAJI NA UTANGAMANO**

Ni muhimu watu kuwajibika katika jamii ili kuleta ufanisi katika jambo lolote lile.Bwawa la Mpingoni lilipoanza kukauka kutokana na mabadiliko ya Hali ya anga,wanajamii wa eneo la kaoleni wanajumuika pamoja kulichimba na kulipanua bwawa Ili kuweza kuhimili mabadiliko ya Hali ya anga.

Mzee Jibril anawajibika katika majukumu yake kama mzazi.Anahakikisha mtoto wake Chale anapokea matibabu kila anapokumbwa na changamoto ya ugonjwa.Anaandamana na mkewe kumpeleka mwanao hospitalini.Chale anapokuwa amelazwa hospitali anamnunilia vitabu vya kusomea na madaftari yakufanyia mazoezi alivyoagiza ili ajiendeleze kimasomo kwa muda alipokuwa pale hospitali.

Mzee Jibril anampatia mwanawe pesa za kutosha za matumizi anapoenda kujiunga na chuo kikuu,"Baba alinipa pesa za kutosha.Nitatumia kiwango fulani kujihakikishia usalama wangu".

4. **UHIFADHI WA MAZINGIRA.**

Ni muhimu kuyatunza mazingira Kwa manufaa yetu na vizazi wenyewe.Wanajamii wa Kaoleni walilitunza Bwawa la Mpingoni kama mboni za macho Yao kwasababu ndilo lililokuwa tumaini lao.


Edit with WPS Office

Walilitumia Kwaanufaa ya mifugo,mimea na kuendeleza desturi walizorithishwa na wazee wao,ikiwemo uogeleaje.kuna haja ya kuyatinza mazingira Kwa kuwa yana manufaa anuwai Kwa binadamu na kutoyatunza vilevile Kuna madhara mzomzo kwao.

5. **ELIMU**

Elimu nikiungo muhimu sana katika maisha ya binadamu.vipawa hufana zaidi vinapoambatanishwa na elimu.mtunzi anadhihirisha wazi kuwa umuhimu wa elimu siwakupigiwa mfano.Chale hakuweza kwenda Bwawani jumamosi Ile Kwa kuwa kaka yake alikuwa na shughuli nyingi za shule ambazo alitaka kukamilisha kabla ya kinyang'anyiro Cha uogeleaji.Kakake Chale anaamua kutoenda bwanani kuogelea kama kawaida yake kwasababu alikuwa na kazi za shule. Hali hii inadhihirisha umuhimu wa elimu na inapaswa kupewa kipau mbele kabla ya jambo lolote.Chale anapolazwa hospitali anamuomba babake amletee vitabu aweze kuendelea na masomo Ili atakaporejea shuleni asipate ameachwa nyuma sana na wenzake.Anajiendeleza kimasomo ijapokuwa Yuko katika Hali na mazingiza tatanishi.Mwuguzi Sudi anakutana na Chale chuo kikuu,kuendeleza taalumu yake.Anaamua kuendelea na masomo ili kuendeleza na kuipiga msasa taaluma yake.

6. **UMUHIMU WA VIFAA VYA KIDIJITALI NA MITANDAO YA KIJAMII.**

Chale anatumia ramani yake kwenye simu yake kujua umbali wa



Edit with WPS Office

anakokwenda.Anaagizia teksi mtandaoni.

7. **DINI**

Ni muhimu Kwa mja yeyote kuwa na Imani ya kidini ambaya huweza kumuongoza katika mienendo yake.Familia ya akina Chale hawakosi sala.Baba Yao ndiye huwaita Kwa Sala ya asubuhi na kila mmoja wao ana siku yake ya kuongoza sala.Sudi anamleta mtumishi wa mungu kumuombea Chale kabla ya kufanyiwa upasuaji.Ni muhimu kumtanguliza mungu mbele katika jambo lolote lile.

8. **MAGONJWA NA ATHARI ZAKE KATIKA AZMA YA BINADAMU.**

Binadamu Huwa na malengo tofauti tafauti ya kujiendeleza kimaisha.Kunao wanaofanikiwa na kunao wanaokosa kufanikiwa kutokana na athari za mangojwa mbalimbali.Licha ya changamoto hizi,binadamu hapaswi kukata tamaa anapougua.Ugonjwa sio mwisho wa azma ya binadamu kuendelea kimaisha.Chale alipokuwa mdogo aliugua ugonjwa wa ukambi.Akapelekwa hospitalini mara ya pili alipougua surua.Mara ya tatu aligua ugonjwa wa kansa na akafanyiwa upasuaji.mbali na kuwa alipitia changamoto nyingi za ndwele ainati,azma yake ya kuwa daktari bado inatimia.binadamu hapaswi kukata tamaa anapougua bali kutafuta tiba na kuendelea na maisha yake.

9. **MABADILIKO**

Duniani Kuna mabadiliko mbalimbali.Hali nyingi duniani si za kudumu milele.Katika novela ya Uteuzi wa Chale,mtunzi



Edit with WPS Office

anadhihirisha mabadiliko mbalimbali.Kuna mabadiliko ya kimazingiza."Awali haikua kawaida kwa bwawa la mpingoni kukauka".Bwawa lilipoanza kukauka ni uthibitisho wazi kuwa maumbile yanachukua sura mpya Kila uchao.Hali ya anga ilikua imebadilika na bwawa kuanza kikauka.

Hospitali kuu ya Kaunti ya Heri ilidhihirisha mabadiliko anuwai.Ukumbi wake ulipanuliwa kiasi.Sheria ziliongezeka zaidi,kutokana na kuibuka Kwa ugonjwa wa Corona,kila mtu alihitajika kukaa mita mbili kutoka Kwa mwenzake.

Vile vile mabadiliko ya kiteknolojia yalidhihirika katika hospitali ya Heri.Usajili wa wagonjwa ulikua tofauti na wa awali.

Kuna mabadiliko ya ki Hali au kimwili.Chale hali take inabadilika.Anaupoteza uzima wake kwa kuugua ugonjwa wa Kansa ambao ulimsababishia kufanyiwa upasuaji na maumbile yake pia kubadilika.Mwendo wake pia unabadilika.anatembea Kwa kuchechemea Kwa kuwa mguu wake mmoja unakua mfupi kias kutokana na athari ya upasuaji.

Chale na familia yake wanabadilika toka hali ya umaskini hadi kuwa tajiri Chale anapokuwa daktari mkuu.

## 10. CHANGAMOTO KATIKA HOSPITALI ZA UMMA.

Katika hospitali za umma,wagonjwa hulazimika kusubiri Kwa muda mrefu kabla ya kuhudumiwa kutokana na mlolongo mkubwa wa wagonjwa na waiguzi au wahudumu  wachache.Wagonjwa hasa wenye maumivu makali huumia zaidi wakisubiri zamu yao



Edit with WPS Office

kufikiwa.Mzee jibril karibu aishiwe na subira katika mlolongo wa wagonjwa akisubiri zamu yake ya kumpeleka mwanawe Kwa mhudumu.Anakosa subira alipouona uso wa mwanawe uliojaa makunyanzi kutokana na uchozi.Vivyo hivyo anakumbuka,subira huvuta heri .

11. **URAFIKI**.

Urafiki baina ya Chale na Sudi unaojengeka hospitalini Sudi akiwa muuguzi wa Chale.Wazoeana Hadi kuwa ndugu wa kufaana.Wanakutatana Tena Chuo kikuu Wakati Chale amejiunga kwa shahada yake ya kwanza ilhali Sudi akiendeleza taaluma yake.

Urafiki baina ya Chale na Dak.Maarifa.

Urafiki baina ya familia ya Chale na Dkt.Maarifa unaotokana na misingi ya kusaidiana.

**12. MAONO KATIKA MAISHA.**

Binadamu lazima awe na maono katika maisha yake.Lazima awe na mipango ya siku zake za usoni.Hawakukosea waliosema safari ya kesho hupangwa Leo.Chale alikuwa na azma yake maishani.Toka alipokuwa mdogo alitaka sana kuwa mtangazaji na alijizatiti vilivyo kuitimiza ndoto yake .Anaposaidiwa na kupona Ugonjwa wa Kansa,anajawa na hamu ya kuwa daktari Ili aweze kuisadia jamii.Anapigania azma yake hadi kuwa yenye ufanisi.Maono yake yanakuwa ya kufana.

13. **KIFO**.



Edit with WPS Office

Vifo vilikuwa dhahiri katika hospitali ya Kaunti ya Heri.Chale alijawa na hofu alipowaona wagonjwa wakipoteza maisha Yao alipokuwa amelazwa katika hospitali hiyo.Kifo ndio kikwazo kikuu Cha azma mbalimbali za binadamu.Binadamu hushindwa kutimiza azma yake anapokumbana na kifo.Chale hakutaka kuipungia Dunia mkono kwa kuwa alikuwa na mambo mengi ya kufanya maishani.

## 14. SUBIRA NA UVUMILIVU MAISHANI.

Binadamu hukumbwa na changamoto anuwai katika maisha yake.Kuna changamoto za magonjwa,Umaskini na kadhalika.

Wazazi wa Chale Pamoja na Chale ni mwenye subra.hawakati tamaa ijapokuwa wanapitia Hali ngumu.wanamatumaini kwamba,kwa kuwa mtoto wao aliweza kuukabili ukambi na surua,angeweza pia kulikabili janga lililomkumba la ugonjwa wa Kansa.Wakiwa katika mlolongo wa wagonjwa hospitalini,wanakuwa wenye subra ijapokuwa mtoto wao aliumia Kwa uchungu.Walijua subra huvuta heri na zamu Yao ingefikiwa.Chale ni mwenye subra.Anapitia changamoto za mangojwa,umaskini ila hakati tamaa maishani.

## 15. KUTOKATA TAMAA.

Binadamu hapaswi kukata tamaa maishani mbali na kuwa maisha yana changamoto anuwai kama vile za maradhi na umaskini.Dhana hii inadhihirika kupitia mhusika Chale ambae mbali nakuwa alikumbwa na changamoto nyingi za magonjwa tangu akiwa mdogo,pamoja na umaskini katika familia,changamoto hizi hazimkatishi tamaa ya kufaulu maishani.Bado anafanikisha ndoto



Edit with WPS Office

yake ya kuwa daktari.Changamoto katika maisha zinafaa kutuongeza ari ya kutaka kupata ufanisi na kujikomboa na wala sio za kutufanya tukate tamaa.

16. **UMASKINI**.

Umaskini ni kikwazo Cha maendeleo ya mja.Binadamu wengi hushindwa kutimiza azma yao maishani kutokana na umaskini.Chale anashindwa kuwaona watangazaji anaowaenzi runingani ili kuwaiga kama njia Moja ya kukikuza kipaji chake Cha utangazaji.Wanakosa Televisheni kwao kutoka na umaskini.Anawasikiliza kijiredioni tu.

Babaka Chale anajawa na hofu baada ya matibabu ya mwanawe kukamilika.Hakuwa na uwezo wakugharamia matibabu Kwa kuwa alijua fika yangekua juu maradufu.

**17. UMAKINIFU KATIKA KAZI.**

Daktari Maarifa anadhihirisha umakinifu mkubwa katika kazi.Hayafuati matibabu ya Chale Kwa pupa.Anafanyia uchunguzi Kwa umakinifu Hadi kupeleka baadhi ya vipimo maabara za ngambo Kwa uchunguzi wa kina.Alipojua bayana tatito la Chale,analieleza kwa wazazi wa Chale kwa umakinifu mkubwa.Katika kumfanyia upasuaji Mgonjwa wake,anakuwa mmakinifu katika kazi yake kuhakikisha kwamba shughuli ile inakua yakufana.Alifanikisha kazi yake kwa kujituma na bila papara na kuyarejesha maisha ya chale



Edit with WPS Office

uzimani.Ni muhimu tusifanye kazi zetu kwa umakinifu na bila papara kwa kuwa kosa dogo tu katika kazi linaweza kusababisha madhara makubwa.

## 18. UTEUZI NA UAMUZI MAISHANI.

Ni vyema binadamu aweze kujifanyia uamuzi mwenyewe katika mustakabali wa maisha yake.Unapofanyiwa uamuzi na mtu wa pili huenda uamuzi huo,usisawiane na kile ukipendacho na hivyo basi kusababisha Changamoto mbeleni.Ijapokuwa tunapaswa kusikiza mawaidha ya watu mbalimbali,katika kufanya maamuzi ni uamuzi wa mtu mwenyewe.Mzee Jibril anamwambia mwanawe Chale ajiamulie mwenyewe kuhusu kipawa ambacho angependa kukiendeleza siku zake za usoni.Japo Chale ana vipawa anuwai kama vile,Utangazaji,Ualimu na Utabibu, anajiamulia mwenyewe ni kipawa kipi angekitilia mkazo zaidi maishani Kwa manufaa ya siku za usoni.Anaamua kusomea udaktari.Chale alipokuwa mngojwa na kuhitajika kufanyiwa upasuaji,anafanya uamuzi mwenyewe.anakubali upasuaji huo japo hafahamu matokeo yake mwishoni yangekuaje.Anatia sahihi kufanyiwa upasuaji.

## 19.MAGONJWA AMBUKIZI,USAMBAZAJI WAKE NA JINSI YA KUJIKINGA.

Ni vyema binadamu kuyafahamu magonjwa mbalimbali yanayomzunguka ili kukabiliana nayo.Wanafunzi katika shule ya Mfinyanzi wanapewa kazi ya utafiti kuhusu magonjwa ambukizi na jinsi ya kujikinga kwayo.Katika uwasilishaji wa utafiti huo,hadhira inajifunza mengi kutoka Kwa utafiti uliofanywa na Chale.Nta zinawatoka masikioni.Ilijifunza kuhusu aina ya magonjwa ya kuambukiza,namna ya kusambaza magonjwa hayo na namna ya



Edit with WPS Office

kujikinga nayo.vilevile wakajifunza mbinu bora za uwasilishaji wa makala .

20. **UONGOZI**.

Jukumu la serikali ni kuhakikisha kuwa inabuni miradi inayowasaidia wananchi  na kupunguza garama ya maisha ya mwananchi.Serikali ya nchi hii iliyokusudiwa inalifanikisha hili kwa kuwajengea wananchi makazi Bora yenye gharama ya chini.Serikali iliwajengea wananchi wake nyumba za ghorofa za bei nafuu kama njia ya kuwahakikishia raia wake makazi bora.Huu ni uongozi bora na wakupigiwa mfano nchini.Serikali hii vile inachukua jukumu la kuzilinda rasilimali za nchi kwa manufaa ya raia.Serikali iliuchunga msitu uliojaa miti pomoni.Ulisheheni aina mbalimbali za wanyamana ndege ambao hawakupatikana katika nchi yeyote.Serikali iliwachukulia hatua watu waliojaribu kuuvamia msitu huu

**21. UHARIBIFU WA MAZINGIRA.**

Watu kujaribu kuuvamia msitu na kuharibu raslimali hii.

Bwawa la mpingoni kukauka kulitokana na mabadiliko ya anga ambayo Kwa kiasi kikubwa husababishwa na uharinifu wa mazingira na mwanadamu.Ni vyema tuyachunge mazingira ili kuepuka athari kama hizi za kukauka kwa sehemu za maji na madhara mengine mengi.

**22. MALEZI.**

Jukumu la wazazi nikuhakikisha watoto wao wanapata malezi bora.Mzee Jibril na Bi.Pili wanalivulia nguo suala hili.Wanahakikisha kuwa watoto wao wanapata elimu hadi kiwango Cha juu zaidi kama



Edit with WPS Office

vile Chale aliyesomea udaktari.Vile vile watoto wao walipokuwa wadogo wanawapatia muda kuweza kujumuika na wenzao katika michezo mbalimbali ili kuhakikisha wanapata wasaa wakuvikuza na kuvipiga msasa vipawa vyao.Vile vile walijua fika kuwa watoto kutangamana na wenzao ni njia Moja ya kukuza ushirikiano baina Yao na pia huweza kuelimishana na kukatazana uovu.

**WAHUSIKA**

1. **CHALE.**

**(a) Mwenye maono**

Akiwa na umri mdogo,Chale alikuwa mwenye azma na maisha yake ya usoni.alikua na azma ya kuwa mtangazaji na alifanya kulihali kuhakikisha azma yake inatimia.Alipobadili nia nakuamua kuwa atasomea udaktari,anatia bidii Hadi ndoto yake kutimia.

**(b) Mwenye bidii**

Anabidii katika kuvikuza vipawa vyake.anabidii masomoni.Anasoma Kwa bidii hadi kuhitimu kuwa daktari.

**(c) Mwenye dini**

Ni muislamu.Hurauka asubuhi kusali na familia yake.Huongoza Sala.Anakubali kuombewa kabla ya kufanyiwa upasuaji

**(d) Mtoto wa Mzee jibril na bi pili**



Edit with WPS Office

Babake ni mzee jibri na mamake bi.Pili

(e)**Jasiri**...sudi alivutiwa na uchangamfu wa chale licha ya uchungu uliouganda mguu wake kama kupe...uk 36

Aliwasilisha kazi yake ya utafiti kuhusu magonjwa ambukizi katika ukumbi wa Mzalendo shule ya Mfinyanzi,mbele ya hadhira Kwa ujasiri.

**(f) Mvumilivu**

Anakuwa mvumilivu anapopitia hali ngumu ya ugonjwa.Anavumilia katika kupata matibabu ambayo yalihitaji kufanywa hatua Kwa hatua na hivyo basi kuhitaji muda wa kutosha.

**(g) Mwenye heshima**

Anawaheshimu wazazi wake,na marafiki zake Sudi na Dkt Maarifa na watu wote katika jamii hiyo ya kaoleni.

(h) **Mwenye hofu/ wasiwasi**...Alijawa na hofu alipokuwa akishuhudia vifo vya wenzake katika wadi aliyokuwa.uk 39

(i) **Mwenye matumaini**...Ana matumaini kuwa atakapo pona ugonjwa wake ataweza kurudi masomoni na kutia bidii Hadi kufanikiwa....uk 52.

(j) **Msomi**...Alihitimu na taaluma ya udaktari wa upasuaji wa Figo.

**2. JIBRIL**

**(a)Babake Chale**

**(b)Mwenye mapenzi ya dhati**



Edit with WPS Office

Anaipenda familia yake

Hakupendezewa na tabia ya mkewe lakini alimsamehe...uk 54.

**(c) Mwenye bidii/kuwajibika.**

Anawajibika katika majukumu mbalimbali ya familia licha ya kipato chake Cha chini.Anawasomesha wanawe,Anashughulikia watoto wake kupata matibabu wanapokuwa wagonjwa.Chale anapohitaji vitabu ili kujiendeleza kimasomo anamnunilia.

**(d) Anaithamini elimu.**

Watoto wake wanaenda shule.

Chale anapojiunga na chuo kikuu anampa pesa za kutosha za matumizi.

Anajizatiti kupata elimu ya ngumbaru.

**(d) mwenye kujali**

Anayathamini maslahi ya familia yake.

**(e)Mwenye dini**...Hufanya ibada na familia yake Kila siku.Hurauka asubuhi kusali.

**(f)Si mvumilivu**...karibu aishiwe na subira alipoutazama uso wa mwanawe...uk 26

**(g)Mvumilivu**...alikumbuka subira huvuta heri...uk 26

**(h)mkulima**...alikuwa ameenda benki kuchukua malipo ya zao lake la mchai....UK 27



Edit with WPS Office

(i)Mpekuzi/mdadisi...

3. **BI.PILI**

(a)**Mwenye mapenzi ya dhati.**..anaipenda na kuijali familia yake.Anaandamana na mumewe kumpeleka mtoto wao hospitalini.

(b) **Mwenye kujali..**."maskini Chale"....alipomuona chale na majeraha ya mguu.

Aliukagua mguu wa mwanawe kuanzia kwenye kifundo Hadi kwenye goti.

Alimchukua mwanawe na kumlaza kwenye kochi.

"Pole Kwa maumivu mwanangu,itabidi tukupeleke hospitali Sasa hivi"....uk 19.

**(c) Mwenye shukrani**

Anamshukuru Daktari Maarifa Kwa msaada mkubwa wa mwanao.

(d) **Mwenye dini**...Hurauka asubuhi nakusali pamoja na familia yake.

(e)Mpekuzi/Mdadisi

4. **SUDI**

(a)**Msomi**...ana taaluma ya uuguzi na mwuuguzi katika hospitali kuu ya kaunti ya heri.

(b) **Mwenye dini**...anamuombea Chale kabla ya upasuaji.



Edit with WPS Office

(c) Mcheshi/Mwenye mzaha.

**(d) Mwenye utu.**

(e)

**5. DKT.MAARIFA.**

**(a) Mwenye maarifa**

Alipokuwa akifanya upasuaji,alitazama kila hatua aliyochukua kuanzia mkato wa kwanza kwenye mguu hadi alipoona tufe lolilokuwa limejificha....uk 56

(b) **Mwenye mzaha**..."Hey young man! Naona umeamka.Hata umeketi!Haikosi hata ulitazama kandanda usiku wa Jana".Daktari maarifa alisema kwa mzaha wake wa kawaida...uk 62

**(c) Mmakinifu katika kazi.**

Wenzake walimtazama tu na kuajabia namna alivyoifanya kazi hii kwa kujituma na bila papara...uk 56

(d) **Mwenye utu**...anasmamia gharama za matibabu ya Chale kuanzia hatua ya kwanza hadi ya mwisho.

(e) **Msomi**...Alihitimu kama daktari wa upasuaji.

**6. WANAJAMII WA KIJIJI CHA KAOLENI.**

(a) **Wenye umoja**...wanaungana pamoja kulichimba bwawa lao ili liweze kukabiliana mabadiliko ya hali ya anga.



Edit with WPS Office

(b) **Watunzaji mazingira/raslimali**...wanalichunga bwawa lao mithili ya mboni za macho Yao.Wanalichimba ili kulipanua liweze kukabiliana na ukame

7. **KAKAKE CHALE.**

**(a) Kakake mkubwa Chale.**

(b) **Anaithamini elimu**...Anakosa kwenda Bwawani Kwa michezo Yao ya kawaida ili kuhakikisha amekamilisha kazi za shule Kwa wakati ufaao...

(c) **Mwenye mapenzi ya dhati**...Anampenda kakake Chale na huandamana naye kuelekea bwawani wakiwa wameshikana mikono.

## MBINU ZA LUGHA.

Ni maneno anayotumia mtunzi katika kazi yake kudhihirisha usanii au ubunifu katika kazi husika.Novela hii imesheni mbinu za lugha kama zifuatazo.

1. **Lakabu**

Majina ya utani yanayotokana na sifa au tabia za mtu au mahali.

(a) Sanduku la Mtangazaji.......uk 1

(b) Mtangazaji mtarajiwa......uk 3

(c) Nyota wa Kaoleni......uk 3

2. **Kisengere nyuma**

Muhusika au mtunzi kusimulia yaliyotokea awali.Masimulizi


Edit with WPS Office

yanawezakuwa Kwa mdomo au kifikra kwa kukumbuka yaliyotokea awali.(a)Mwandishi kusimulia hali ya  awali ya bwawa la mpingoni ya kwamba haikuwa kawaida yake kukauka....uk 1

(b) Mwandishi anarejelea Bi Pili ambae alipomtazama mwanawe Chale ambaye alikua amefura mguu na joto kuzidi anakumbuka mara ya mwisho alipomwona mwanawe katika hali hiyo.Anakumbuka nyuma mwanawe alipougua Surua.....uk 18

(c) Mwandishi akirejelea Bi Pili ambaye anayakumbuka mengi yaliyopita anapokaribia lango kuu la hospitali.Anakumbuka kuwa pale ndipo alipojifungua Chale,na kuwa hapo ndipo nusura ampoteze mwanawe Kwa ukambi. Wanakumbuka walivyoandamana na mumewe kumleta chale hospitalini alipougua surua....uk 25.

3. **Uhuishi/Tashihisi.**

Kukipatia sifa ya uhai au ya ubinadamu kisichokuwa binadamu.

(a) Bwawa la Mpingoni lilisimama hapo tangu zamani...uk 1

(b) Bwawa lilijikita Kwa mbwembwe kando ya mto kaumu...uk 1

(c) Mguu wake ulikuwa umemfunga kwenye wadi hii bila kumwambia sababu za kumfunga....uk 39



Edit with WPS Office

(d) Machela ilijitandaza Kwa dharau machoni mwa Jibril na mkewe....uk 53

(e) Ukumbi wa Mzalendo katika shule ya Mfinyanzi ulijaa na kitapika wanafunzi ....uk 74

4. **Tashbihi**

Ulinganisho wa moja Kwa Moja unaotumia viunganishi,kama,mithili,ja,mfano wa ...n.k

(a) Lilikaidi misimu mingi ya kiangazi chenye joto Kali kama moto wa tanuri....uk 1

(b) Alikua akiogelea kama samaki...uk 3

(c) Wako tayari wanasubiri kipenga ili wajitome majini kama papa...uk 6

(d) Yalipotua kwenye mguu wake wa kulia,yaliganda hapo kama jokofu....12.

5. **Taswira**

Picha inayojengeka akilini mwa msomaji anaposoma kazi Fulani ya uandishi.

(a) Chale akiwa na umri wa mitatu angeandamana na kaka yake asubuhi.Angeketi ukingoni mwa bwawa huku kaka yake akimshika mkono.Angevitia viguu vyake kwenye maji na kuvichezesha humo.....uk 3

(b) Bi pili aliamua kuukagua Tena mguu wa Chale kuanzia kwenye kifundo hadi kwenye goti.Alikishika kifundo na



Edit with WPS Office

kukitomasa.Karibu Chale afyatuke kama mshale kutoka kwenye kochi alilokua amekalia....uk 14.

(c) Chale katika chumba Cha upasuaji akifanyiwa upasuaji.

(d) Dkt.Maarifa katika chumba Cha upasuaji akifanyiwa upasuaji.

(e) Chale akiwasilisha Kazi yake ya utafiti kuhusu magonjwa ambukizi katika ukumbi wa mzalendo shule ya mfinyanzi...uk 74

**6. Maswali balagha**

Maswali ya balagha ni maswali ambayo msimulizi au mhusika hujiuliza bila kutarajia jibu. Umuhimu wa maswali haya ni kuchochea fikira za hadhira. Pia huitwa mubalagha, tashititi, tashtiti . Rhetorical Questions . Maswali haya yanaweza kujitokeza katika uzungumzi nafsia ambapo mhusika hujiongelesha kana kwamba anazungumza na mtu mwengine.

(a) "Itakuaje mtoto ashabihiane na babake si kwa sura tu Bali pia kitabia?".....uk 3.

(b) Au huenda niligonga jiwe wakati nilipokuwa nikitoka baba alipokuja?....uk 11

(c) Au niliumwa na konokono?....uk 11

(d) Lakini hao konokono wanatoka wapi?....uk 11

(e) Angewaambia nini na alipoenda kulala alijawa na bashasha na ucheshi wake wa kawaida?



Edit with WPS Office

(f) Je wakati huu heri itawafuata au wataandamwa na Shari?...uk 25.

7. **Uzungumzi nafsia**.

Uzungumzaji nafsia (nafsiya) ni pale mhusika anapojizungumzia mwenyewe kana kwamba anaongea na mtu mwengine. Uzungumzaji huu hutumika kuonyesha mtiririko wa mawazo katika akili ya mhusika. Monologue

(a)"Kwa kweli mwana wa muhunzi asiposana huvuvia.Itakuaje mtoto ashabihiane na babake si kwa sura tu bali pia kitabia?"-mzee jibril...uk 3

(b) Pengine nikiendelea kufanya bidii katika utangazaji huenda nitawavutia wengi.Si lazima ningoje hadi ndoto yangu ya kuwa mtangazaji katika shirika la utangazaji itimie"-Chale...uk 4

(c)"Ni kana kwamba hawa watangazaji wanatujua sisi ambao hatujafikia kiwango cha kuyaelewa mengi."-Chale...uk 4.

8. **Tabaini**.

Mwandishi kutumia neno si kudhihirisha msisitizo katika kufanya au kufanyika Kwa jambo.Ikumbukwe kuwa, si katika tabaini haidhihirishi kukataa jambo bali kuonyesha msisitizo au kiwango Cha kufanyika Kwa jambo Fulani.

(a)Alifungua stesheni hii na ile.Akasikiliza mtangazaji huyu na yule.Si wa taarifa ya habari,si wa matangazo maalum,si wa michezo....uk 4.

(b) Alikuwa amefanyiwa uchunguzi huu na ule.Si wa viungo



Edit with WPS Office

vya ndani vya mwili,si wa damu,si wa haja kubwa na ndogo,si eksirei maalum ya kifua....uk 36.

(c) Kusomea chuoni si mchezo...uk 84.

**9. Takriri**

Urudiaji wa neno au kifungu cha maneno ili kuonyesha msisitizo.

(a) Hivi ndivyo walivyoandamana wakati walipomtoa Chale hospitalini akiwa kilaika.Hivi ndivyo walivyoandamana wakati walipomleta hospitalini alipougua surua.Hivi ndivyo walivyoandamana waliporuhusiwa kwenda nyumbani baada ya tabibu kuwaokolea mwanao kutokana na ugonjwa huo hatari wa kuambukiza...uk 25

(b) Hakujua kias Cha uchungu ulomwandama mwanawe.Hakujua kwamba chale asingeweza kujiinua hata kidogo.Hakujua kwamba kuanzia siku hiyo,Chale angekua akiwategemea wengine kumtoa hapa hadi pale.Hakujua kwamba mustakabali wa elimu ya mwanawe ulikuwa umegibikwa gubigubi na wingu la mashaka....uk 35

**10. Sitiari**

Ulinganisho wa Moja Kwa moja usiotumia viunganishi.

(a) Runinga ni nguo ya kuazima....uk 4

(b) Hata hivyo alijipa moyo kwa kujiambia kwamba Chale alikua jabali....uk 52.

**11. Msemo**

Misemo ni kauli fupifupi zinazotumiwa na jamii ili kusisitiza ukweli



Edit with WPS Office

wa jambo fulani. Ni mafungu ya maneno ambayo hutumiwa na jamii fulani kwa lengo la kutoa msisitizo wa maadili fulani.Misemo huunganisha dhana au mawazo mawili kuwa moja.

(a)Nguo ya kuazima haikidhi haja...uk 5

(b) Leo ni Leo msema kesho ni mwongo...uk 5

(c)Usione wembamba wa reli...uk 6

(d) Safari ndefu huanza kwa hatua moja....uk 11

(e)Wasiwasi uliadimika kwake kama maziwa ya kuku...uk 15

(f) Penye nia pana njia...uk 40

(g)Liandikwalo halifutiki...uk 53

(h) Lisilobudi hutendwa...uk 54

(i) Haya ni maji ambayo alikua ameyavulia nguo...54

(j) Milima tu ndiyo haikutani...uk 86

**12. Utohozi**

Utohozi (kutoka kitenzi "kutohoa") ni kitendo cha lugha fulani kukopa maneno ya lugha nyingine kwa kuyapatia tu matamshi rahisi kwa wenyeji bila ya kuyatafsiri.

Kutohoa nikuswahilisha neno.Yaani neno kutoka lugha ngeni kama kingezereza kulibadilisha kimatamshi ili kukidhi mahitaji ya kiswahili bila ya kulitafasiri.

**(a)** Televisheni kutoka neno television...uk 5



Edit with WPS Office

(b) Kaunti kutoka neno county....uk 5

(c) Nesi kutoka neno nurse...uk 19

(d) Stethoskopu kutoka neno stethoscope...uk 22

(e) Eksirei kutoka neno X-ray...uk 28

(f) Faili kutoka neno file uk 29

(g) Thieta kutoka neno theater...uk47

**13. Nahau**

Nahau ni semi fupifupi ambazo hutumia lugha/maneno ya kawaida lakini maneno hayo hutoa maana tofauti na ile iliyo kwenye maneno ya awali.

(a) Kuwatupia jicho- yaani kuwachunga...uk 5

(b) Inampiga chenga-yaani ngumu kupatikana...uk 15

(c) Moyo wa jabali- yaani moyo thabiti,wenye msimamo,moyo usio na hofu....uk 15

(d) Shingo upande-kutoridhika...uk 16

(e) Kubwabwaja maneno- kuongea bila kusita...uk 17

(f) Kuchungulia kaburi-karibia kifo...uk 18

(g) Ilimletea mwanga-kumfungua akili...uk 27

(h) Maji yalizidi unga-...uk 37

(i) Anamtupia jicho-kumtazama....uk 37



Edit with WPS Office

(j) Nikasalimu amri-kukubali...uk 39

(k)Kufanya juu chini-kila Hali...39

(l) Kuzitemea mate-...uk39

(m) Kuipungia Dunia mkono-kufariki...uk 40

(n) Kumpiga jeki-kumsaidia...uk 51

(o)

**14. Methali**

Ni kauli fupi yenye pande mbili za fikra, ambazo upande wa kwanza huanza upande wa pili humaliza. Kwa mfano: Mficha ugonjwa, kifo humuumbua. Mcheza kwao hutunzwa. Haraka haraka haina baraka. Mkono mtupu haulambwi. Mkamia maji hayanywi.

(a)Asiyesikia la mkuu huvunjika guu....uk 11

(b) Uchungu wa mwana aujuaye ni mzazi....UK 13

(c)Subira huvuta heri....26

(d) Haraka haraka Haina baraka...uk 45

**15. Mdokezo**

Mdokezo ni tamathali ambayo hudokeza kitu fulani na kukiacha bila kukikamilisha kwa maana ya kwamba kinaweza kukamilishwa na mtu mwingine kisanaa.



Edit with WPS Office

(a)Usione wembamba wa reli...UK 6

**16. Msamiati**

(a)Hulka-tabia...uk

(b)

**17. Chuku**

Chuku ni kutumia maneno yaliyotiliwa chumvi ili kusisitiza ujumbe fulani au kusifia kitu.

(a)Kama alivyokuwa ametabiri,macho ya babake yalipenya Hadi moyoni mwake...uk12

(b) Yalimpekua Chale toka kuanzia utosini hadi moyoni mwake...uk 12.

(c)Ilikuwa miti mirefu karibu kufikia mbingu...uk 81

(d) Wakati huo hata nafasi ya kutema mate haikuwepo...uk 81

**18. Sadfa**

Sadfa ni kugongana kwa vitendo viwili vinavyohusiana kana kwamba vilikuwa vimepangwa, japo havikuwa vimepangiwa

(a)"jamani, Chale! Mguu una Nini?"Mzee jibril na mkewe walitamka Kwa pamoja kana kwamba walikuwa wamefanya mazoezi ya kauli ambayo wangemtolea mtoto wao...uk 13.

(b) Chale ambaye anapenda utangazaji anapofika hospitali analazwa katika chumba Kilichokuwa na runinga.Alikuwa ameinzi Kwa kuwa nyumbani kwao hawakuwa nayo...uk 31

(c)Chale anakutana na rafikiye wa dhati na mwuguzi wake sudi



Edit with WPS Office

chuoni.Walikuwa wamezoea si kama mgonjwa na mwuguzi wake tu bali kama ndugu wa toka nitoke.walisaidiana Kwa mengi yosiyoweza kuhesabaika Katika hospitali ya Kaunti ya Heri Chale alipokuwa amelazwa.Wanatengana Chale anapotoka hospitali lakini Kwa kuwa ya mungu ni mengi wanakutanishwa tena chuo kikuu....uk 84

(d) Ni sadfa kuwa Daktari Maarifa alimsaidia Chale ili naye aje asaidiwe maisha yake na Chale...94

19. **Kuhamisha ndimi**

Ni kuingiza sentensi ya lugha nyingine katika kifungu cha lugha ya Kiswahili. Kinyume na Kuchanganya ndimi (ambapo mwandishi huchanganya maneno katika sentensi moja, katika kuhamisha ndimi, sentensi kamilifu ya lugha nyingine hutumika miongoni mwa sentensi za Kiswahili sanifu.

(a)"Ouch!Ouch!Chale alilia Kwa uchungu...uk14

(b) "Hey young man!"Daktari maarifa alisema Kwa uchangamfu...uk62

(c)"Hey Doc,alisema Chale....uk 70

(d) "Excuse us.We are very sorry.We got carried away"

(e)The operation was successful.sasa umepina,Mzee wangu...uk 94



Edit with WPS Office

## 20. Kuchanganya ndimi

Kuchanganya ndimi ni mbinu inayotumiwa na mwandishi kuonyesha hali ya kuzungumza lugha mbili au zaidi kwa pamoja katika sentensi moja.

(a)"Vipi Boss?Uliweza kukitazama kile kinyang'anyiro Cha soka Cha saa nne usiku?"

(b) Huyu ni miongoni mwa wale ambao watu huita Gifted and talented...UK 63

(c)"Je,Doc,mtu anaweza kuwa daktari na wakati huohuo akawa mtangazaji....UK 70.

(d) Chale alisomea tiba ya jumla,akahitimu kama physician...uk87

## 21. Taashira

Ni matumizi ya lugha ya ishara kuwakilisha ujumbe fulani. Jina au kitu fulani kinatumika hali fulani yenye uhusiano na kile kilichotumiwa. Vitu vinayotumika katika taashira ni vitu vinavyofahamika na watu wengi kwa ujumla kuwa na uhusiano na hali inayowakilishwa.

(a)Chale kuugua ugonjwa wa ukambi na surua alipokuwa mtoto na akafanikiwa kupona ilikuwa  ishara njema ya kuwa hata ugonjwa wa kansa uliompata angeweza kupona...UK 25



Edit with WPS Office

(b) Vipaji alivyomiliki Chale toka utotoni na kuhakikisha anaviendeleza mbali na changamoto zilizomkumbwa ilikuwa ishara tosha ya kwamba angefanikiwa maishani.

(c) Machozi ya Bi.Pili mamake Chale ilikuwa ishara ya habari mbaya za mwanawe...Na Kweli chale alipatikana na Kansa.

(d) Watu walioisukuma machela walivali Makoti ya rangi ya kijani kibichi.

**22. Majazi**

Majazi ni mbinu ya mhusika kuwa na jina lake rasmi (jina la kuzaliwa) linaloambatana na tabia/mienendo/sifa zake. Aidha, majazi inaweza kuwa mbinu ya sanaa.

(a) Dkt.Maarifa ana ujuzi(maarifa) wa hali ya juu katika taaluma.Anamfanyia Chale upasuaji na kumtoa seli zinazosababisha uvimbe wa Kansa.Anadhihirisha ujuzi na umakinifu(maarifa katika kazi yake)

(b) Hospitali kuu ya Kaunti ya Heri

(c) Mji wa Tukasake...kusaka elimu ya afya na tiba....uk78

(d) Ufukwe wa shangwe....uk87

23. **Jazanda.**

Ni kulinganisha vitu viwili moja kwa moja bila kutumia viunganishi..

Tofauti kuu kati ya Jazanda na Istiara ni kwamba isitiara hulinganisha kwa kutumia kiungo "ni" ilhali jazanda haitumii



Edit with WPS Office

kiungo chochote.

Kwa mfano:

Isitiara: - Mke wa Bwana Ali ni kasuku.

Jazanda: - Bwana Ali alioa Kasuku...

Katika novela hii mbinu hii imedhihirika kama ifuatavyo

(a)Alimshukuru sana na kumpongeza Chale kwa kutokata tamaa hata wakati ambapo uzi ulioyaunganisha maisha yake ulikuwa karibu kukatika...uk 70.



Edit with WPS Office